Ukubwa wa kaya na namna zilivyo

Karibu asilimia 14 ya watoto wenye umri wa miaka 15 ni watoto wa kufikia- hii ina maana kuwa watoto hawa wanaishi kwenye kaya bila ya wazazi wao waliowazaa. Kufuatana na kiwango kikubwa cha ukimwi Tanzania, kiwango hiki kinaweza kukuwa hapo baadae. Asilimia moja ya watoto ni yatima (wazazi wao wote waliowazaa wameshafariki) na asilimia tisa wamepoteza mama au baba.

Aina ya nyumba

Hali ya nyumba inatuonyesha kiwango cha ustawi wa jamii na uchumi wa kaya na ni kichocheo cha hali ya afya ya wana kaya. Ingawa kuna asilimia 8 ya kaya zenye umeme kuna tofauti kubwa kati ya mijini na vijijini, ambapo aslimia 27 ya kaya za mijini zina umeme wakati asilimia 1 tu ya kaya za vijijini zina umeme. Kwa ujumla theluthi mbili ya kaya zina maji safi ya kunywa. Watu wanaoishi maeneo ya mijini wanapata huduma ya vianzo vya maji safi kuliko watu wanaoishi maenao ya vijijini (asilimia 92 kwa 56). Inawachukuwa dakika nne tu kwa wakazi wa mijini kufika kwenye vyanzo vya maji, ukilinganisha na nusu saa kwa wakazi wa vijijini. Kaya tisa kati ya kumi wanatumia vyoo vya shimo, kukiwa tofauti ndogo kati ya mijini na vijijini. Mwisho, kaya nane kati ya kumi, nyingi zikiwa vijijini, wanaishi kwenye nyumba zilizosakafiwa na udongo au mchanga. Utumiaji wa saruji kwa kusakafia unaonekana zaidi maeneo ya mijini (asilimia 63) kuliko maeneo ya vijijini (asilimia 6).

Idadi ya watu na namna walivyo



Umiliki wa vifaa vya kudumu

Kumiliki vifaa vya kudumu kunaonekana zaidi maeneo ya mijini kuliko vijijini. Kwa mfano, asilimia 73 ya kaya za mijini zinamiliki angalau moja ya vifaa vifuatavyo: redio, luninga (TV), jokofu, baiskeli, pikipiki, au gari la binafsi au lori, ukilinganisha na asilimia 50 ya kaya za vijijini. Vifaa vya aina mbili vinavyomilikiwa zaidi ni redio (asilimia 43 kwa nchi nzima) na baiskeli (asilimia 32). Kwa vifaa vingine, ni asilimia 2 ya kaya au chini ya hapo zinamiliki mojawapo ya vifaa hivyo.

Kiwango cha elimu cha wanawake na wanaume

Elimu ni jambo muhimu katika kuinuwa hali ya kinamama na watoto wao. Matokeo ya utafiti yanaonyesha kuwa asilimia 36 ya wanawake wenye umri wa miaka 15 - 49 na asilimia 22 ya wanaume wenye umri wa miaka 15-59 hawajui kusoma kabisa. Wanawake wa mijini na wanaume wameelimika zaidi kuliko wenzao wanaoishi vijijini. Kwa kiwango cha elimu, zaidi ya nusu ya wanawake (asilimia 52) wamemaliza elimu ya msingi au zaidi, wakati asilimia 27 hawana elimu kabisa. Kwa wanaume asilimia 58 wana elimu ya msingi au zaidi na asilimia 14 hawana elimu kabisa.

UZAZI

Uzazi ulivyo hivi sasa na mwenendo wake

Kwa hali ya uzazi ilivyo sasa hivi, Mwanamke wa Tanzania anazaa kwa wastani wa watoto 5.6 katika kipindi chote cha uzazi. Kiwango hiki kinaonyesha kushuka kidogo kutoka watoto 5.8 kwa kila mwanamke kama kilivyojionyesha katika utafiti wa 1996 TDHS na kushuka kwa mtoto mmoja kama kilivyokuwa katika takwimu za sensa ya watu ya Tanzania ya mwaka 1988.

Wanawake wanaoishi maeneo ya vijijini (kwa wastani wa watoto 6.5) wana watoto watatu zaidi ya wenzao wa mijini (watoto 3.2). wanawake wanaoishi Tanzania Bara wana watoto sawa kama wenzao wa Zanzibar (watoto 5.6). Uzazi unahusiana zaidi na kiwango cha elimu ya mama. Wanawake wasioelimika wana wastani wa watoto 6.5, wale wasiomaliza elimu ya msingi wana watoto 5.1, na wanawake waliomaliza elimu ya msingi au waliopata elimu ya juu wana wastani wa watoto 4.9.

Matatizo ya afya ya kina mama na watoto yanaongezeka wakati watoto wanapozaliwa na kina mama wenye umri mdogo. Mmoja kati ya Watanzania wanne wanapofikia umri wa miaka 17 tayari wameshakuwa na watoto (asilimia 17) au tayari ana mtoto mmoja wakati akiwa na mimba (asilimia 8). Idadi inaongezeka na kufikia asilimia 46 kwa kina mama wanapofikia umri wa miaka 18. Mimba zinazopatikana kwa kina mama wenye umri mdogo na uzazi kwa kina mama wadogo una kiwango kikubwa kwa Bara (asilimia 25) kuliko Zanzibar (asilimia 17) lakini hautofautiani sana kwa mahali wanapoishi (mijini: asilimia 23, vijijini: asilimia 25)

Ndoa na inavyojitokeza kupata uja uzito

Umri wa kuolewa au kukutana kimwili kwa mara ya kwanza ni vitu muhimu vinvyowafanya wanawake wapate mimba. Kwa ujumla, wanawamke wanao olewa mapema wanakawaida ya kuzaa mapema na kuwa na watoto wengi kuliko wanao chelewa kuolewa. Kawaida hii ni ya ukweli kwa Tanzania ambapo matumizi ya njia za uzazi wa mpango bado hazijawafikia wanawake wengi. Nusu ya wanawake wenye umri wa miaka 25-49 wameolewa wakiwa na umri wa miaka 18.1 wakati wanaume wanachelewa kuoa mpaka wafikie umri wa miaka 23.7 - tofauti ya zaidi ya miaka mitano. Wanawake wa vijijini, wanawake wa Zanzibar na wanawake wenye elimu zaidi wanachelewa kuolewa.

Ingawa wastani (median) wa umri ambao mwanamke anakutana kimwili (asilimia 16.6 kwa ujumla) inatofautiana kidogo kufuatana na mahali wanapoishi. Kuna tofauti kubwa kwa wanaume. Kwa mfano wanaume kutoka Bara kwa mara ya kwanza wanakutana kimwili wakiwa na umri wa miaka 17.8, wakati wale wanaoishi Zanzibar wanasubiri mpaka wanapofikia umri wa miak 21 ndiyo wanapoanza kukutana kimwili. Wanawake wasiyokuwa na elimu wanakutana kimwili kwa mara ya kwanza wakiwa na umri wa miaka 15.8 wakati wale wenye elimu ya sekondari wanasubiri hadi wanapofikia umri wa miaka 18.8. Tofauti haijionyeshi sana kwa wanaume (miaka 17.4 kwa wasiyo na elimu na miaka 18.5 kwa wenye elimu ya sekondari).

Vipindi vya uzazi

Watoto wengi (asilimia 83) Tanzania wanazaliwa baada ya kile kinachoitwa kipindi salama - miezi 24 au zaidi kati ya mtoto mmoja na mwengine. Watoto wanaozaliwa kati ya vipindi vifupi wanakuwa katika hali ya hatari kupoteza maisha, halikadhalika na kina mama. Wastani (median) muda kati ya mtoto na mtoto kuzaliwa ni miezi 33 kwa nchi nzima, ni miezi saba pungufu kwa wale wenye watoto ambao mtoto aliyemtangulia amefariki kuliko wale ambao mtoto aliyemtangulia yu hai.

Kupendelea aina ya watoto

Kwa kawaida wanawake wa Tanzania wanapendelea familia ndogo kuliko walizo nazo. Laiti wanawake wangekuwa na idadi ya watoto wanaopendelea, wangekuwa na wastani wa watoto waliozaa 4.8. Idadi hii ni karibu mtoto mmoja pungufu kulingana na wastani uliopo hivi sasa.

Wanawake wanaoishi maeneo ya mijini, wale wanaoishi Zanzibar na wale waliyomaliza elimu ya msingi wanaelekea kuwa na hali nzuri ya kufahamu idadi ya watoto wanaopendelea kuwa nao. Kwa mfano, wanawake wa mijini wanataka watoto 2.9, ni pungufu kidogo kuliko uzazi halisi wa watoto 3.2 waliyokuwa nao. Kwa upande mwengine, wanawake wa vijijini wanaozaa watoto 6.5 wanapendelea kuwa na watoto 5.5- tofauti hii ni kubwa.

Uzazi na kupendelea watoto





Kwa ujumla, mwanamke mmoja kati ya wanne wenye uwezo wa kuzaa anasema hataki tena mtoto. Mahitaji ya wanawake katika kupunguza watoto wanaozaa yanatofautiana sana kufuatana na wanapoishi na elimu. Asilimia 17 ya wanawake wa Pemba hawahitaji tena watoto zaidi, wanawake wa vijijini wa Bara (asilimia 26) na wanawake wa mijini (asilimia 24) wanaonesha kupendelea kwa hali ya juu kupunguza idadi ya wanaozaa. Wanawake wasiyo na elimu (asilimia 32) na wale ambao hawakumaliza elimu ya msingi (asilimia 26) hawana nia ya kutaka kutokuwa na watoto zaidi.

Kwa ujumla, zaidi ya mtoto mmoja kwa kila watoto watano wanaozaliwa Tanzania hawakupangwa kuzaliwa; asilimia 11 walitaka kuzaliwa baadae na asilimia 11 hawakutakiwa kuzaliwa. Watoto ambao hakutakiwa kuzaliwa ni wengi kwa wanawake wenye umri wa miaka ya 40 (asilimia 30). Kufuatana na wanawake wengi ambao tayari wameshakuwa na watoto wengi, wamekuwa katika hatari zaidi ya kupata maradhi yatokanayo na uzazi na watoto wao pia wapo katika hatari ya kupoteza maisha, hatua madhubuti zinahitajika kuchukuliwa kuwawezesha kupatiwa njia nzuri za kurekibisha uzazi.

Uzazi wa Mpango

Kufahamu na kukubali njia za uzazi wa mpango

Kufahamu na kukubali njia za uzazi wa mpango kumesambaa kwa wanawake na wanaume wa Tanzania wenye umri wa kuweza kuzaa. Zaidi ya wanawake na wanaume tisa kwa kila kumi wanajua njia moja ya kisasa ya uzazi wa mpango. Njia ya vidonge inafahamika zaidi na wanawake (asilimia 86 ukilinganisha na asilimia 79 ya wanaume), wanaume wanafahamu zaidi njia ya mpira wa baba (asilimia 90 kulinganisha na asilimia 83 ya wanawake). Kufahamu njia ya vidonge kunazidi kuongezeka. Asilimia ya wanawake waliosikia njia ya kisasa ya uzazi wa mpango imeongezeka kutoka asilimia 72 mwaka 1991-92 hadi asilimia 84 mwaka 1996 na asilimia 91 mwaka 1999. Halikadhalika, matokeo ya hivi sasa yanaonyesha mbili ya tatu ya Watanzania wanaoishi pamoja (mke na mume) wanakubaliana na njia za uzazi wa mpango.

Kuna njia nyingi nzuri za kuweza kuwafahamisha kina mama na kina baba kuhusu uzazi wa mpango na kukuza utumiaji wake. Njia moja wapo ni wafanyakazi wa sehemu zinazotoa huduma za afya kuzungumza na wasiotumia njia yoyote kuhusu njia mbali mbali kwa ajili ya kurekibisha namna ya kupata watoto. Katika kipindi cha miezi 12 kabla ya utafiti, asilimia 53 ya wasiyotumia njia yoyote ya uzazi wa mpango wamehudhuria sehemu zitoazo huduma za afya (kwa sababu moja ama nyingine). Ni mmoja kati ya watatu wamesema kuwa mtu mmoja ambae ameongea nao kuhusu uzazi wa mpango. Halikadhalika, asilimia 5 ya wasioyotumia njia yoyote wametembelewa na mfanyakazi wa uzazi wa mpango katika kipindi hicho.

Kuwa wazi na taarifa za uzazi wa mpango

Zaidi ya sekta ya afya, waandishi wa habari, ngoma na njia nyingine za kukuza utumiaji wa uzazi wa mpango ni vyanzo muhimu vya habari kuhusu suala hilo. Hata hivyo, saba ya kumi ya wanaume wameripotiwa kuwa wamesikia au wameiona njia mojawapo ya uzazi wa mpango katika kipindi cha miezi sita iliyopita. Redio ni chanzo muhimu (asilimia 42 ya wanawake na asilimia 57 ya wanaume), ikifuatiwa na mabango makubwa (bill-boards) (asilimia 24 na 33) na mabango (asilimia 29 na 29). Uwazi wa programu za afya ya jamii kwenye redio unaongezeka. Kwa mfano, asilimia ya wanawake waliowahi kusikiliza mchezo wa Zinduka katika kipindi cha miezi sita kabla ya utafiti imeongezeka kutoka asilimia 25 mwaka 1996 hadi asilimia 34 mwaka 1999.

Matumizi ya hivi sasa ya uzazi wa mpango kwa njia (wanawake wote wenye umri wa 15 - 49)



Utumiaji ulivyo hivi sasa na mwenendo wake

Wakati asilimia 41 ya wanawake na asilimia 48 ya wanaume wanasema wameshawahi kutumia njia ya uzazi wa mpango, matumizi yalivyo hivi sasa ni

karibu nusu ya asilimia hiyo (asilimia 22 kwa wanawake na asilimia 29 kwa wanaume). Matumizi ya njia za kisasa ni asilimia 16 kwa wanawake na asilimia 21 kwa wanaume. Njia ya sindano na vidonge (zote zikiwa na asilimia 5 kila moja) ni njia ambazo zinatumika sana na wanawake; matumizi ya mpira ni ya tatu kutumika ikiwa na asilimia 4. Kwa wanaume mpira ni chaguo lao lenye asilimia 12 kulinganisha na asilimia 4 waliotoa taarifa ya wenza wao kutumia vidonge.

Matumizi ya hivi sasa ya njia yoyote ya uzazi wa mpango kwa



Kuna tofauti kubwa kwa matumizi ya hivi sasa kufuatana na mahali wanapoishi na kiwango cha elimu. Asilimia ishirini na tatu ya wanawake wa Bara kwa hivi sasa wanatumia njia ya uzazi wa mpango (asilimia 33 ya wanaoishi mijini na asilimia 18 ya wanaoishi vijijini), kulinganishwa na Zanzibar (asilimia 7 kwa Pemba na asilimia 19 kwa Unguja). Elimu pia inachukuwa umuhimu wake: asilimia 14 ya wanawake wasio kuwa na elimu hivi sasa wanatumia njia ya uzazi wa mpango, kulinganisha na asilimia 43 waliokuwa na elimu ya sekondari au zaidi. Ingawa matumizi ya hivi sasa ni makubwa kwa wanaume, inaonyesha kuwa sawa na wanawake kwa kijiografia na elimu.

Zaidi ya nusu (asilimia 55) ya wanawake na wanaume wa Tanzania ambao hawatumii njia ya uzazi wa mpango wameeleza kuwa hawana nia ya njia yoyote kwa kipindi cha miezi 12 ijayo. Kati ya wanaume, sababu kubwa ya kutotumia ni kuwa bado hawajaoa. Sababu nyingine muhimu kwa wanaume na wanawake ni kutaka watoto zaidi au hawakubaliani na njia za uzazi wa mpango.

Vyanzo vya njia za kisasa

Wanawake wawili katika kila wanawake watatu wanaotumia njia za kisasa wanazipata kutoka sekta za umma (serikali), nazo ni, zahanati (asilimia 27), vituo vya afya vya serikali (asilimia 18), hospitali za wilaya (asilimia 13) na hospitali za mikoa (asilimia 8). Sekta za binafsi (hasa maduka ya dawa ni asilimia 10) wanatoa asilimia 22 ya nia za kisasa, wakati maduka (asilimia 6) na marafiki na ndugu (asilimia 4). Wanawake wanaotumia vidonge, sindano na kufunga kizazi kwa kinamama wanategemea sana huduma za umma, wakati mpira wa baba unategemewa sana kutoka kwenye sekta za binafsi (maduka ya dawa, maduka, na marafiki na ndugu).

Kuhitaji uzazi wa mpango

Karibu kila mwanamke mmoja kati ya wanawake watano walio olewa (asilimia 22) hawataki mtoto mwengine au wanataka kucheleweshe kupata mimba lakini hawatumii njia yoyote ya uzazi wa mpango ili kutimiza lengo lao. Kiwango cha wanaotaka kutumia njia za uzazi wa mpango lakini hawazipati kimekuwa kikipunguwa kuanzia mwaka 1991-92, ilipokuwa asilimia 30. Kwa upande mwengine, mahitaji halisi yanayotosheleza yamekuwa yakiongezeka sana, kutoka asilimia 26 mwaka 1991-92 kufikia asilimia 44 mwaka 1996 hadi asilimia 54 mwaka 1999.

UZAZI NA AFYA YA UZAZI

Huduma za uzazi

Huduma za uzazi kutoka kwa wataalam wa afya zimesambaa Tanzania: kina mama wanapata huduma hizo kwa zaidi ya kila watoto tisa kati ya kumi wanaozaliwa. Wahudumu wa afya (health aides) (asilimia 44) wanatoa huduma nyingi, ingawa mafunzo waliopata si makubwa ikilinganishwa na manesi na wakunga wanaotoa asilimia 43 ya huduma za uzazi. Wanawake wenye elimu kubwa (asilimia 24), wale wanaoishi maeneo ya mijini (asilimia 15), na wale wanaoishi Unguja (asilimia 11) ndiyo wanaokwenda zaidi kuonana na madaktari kwa ajili ya huduma wakati wakiwa na mimba. Kwa upande mwengine, wanawake wanaoishi vijijini (asilimia 3), wanawake wanaoishi Pemba (asilimia 2) na wanawake wasiokuwa na elimu (asilimia 2) ni wachache wanaowaona madaktari. Kwa ujumla, asilimia 70 ya wanawake wamehudhuria kwenye huduma za afya mara nne au zaidi wakati wakiwa na mimba, mara ya kwanza wakiwa na mimba ya miezi mitano au sita, ni muda mrefu kuliko inavyopendekezwa.

Wanawake wanne kati ya kumi walipohudhuria kwenye huduma za afya waliambiwa ishara zinazotokana na matatizo ya mimba. Kwa mfano, zaidi ya nusu ya wanawake walifahamu kuwa homa inaweza ikawa ni dalili ya matatizo ya mimba, na mwanamke mmoja kwa kila watatu walisema kuwa kutokwa na damu nyingi ni ishara ya kuwa mwanamke mwenye mimba anahitaji msaada wa kitaalam.

Mambo mengine yanayohusu huduma wakati mwanamke akiwa na mimba yalichambuliwa: asilimia 44 ya wanawake wamesema wamepewa au wamenunua vidonge vyenye madini chuma (iron tablets), wakati asilimia 32 wamesema hivyo hivyo kwa vidonge vya kuzuia ugonjwa wa malaria. Asilimia 83 ya wanawake (kulinganisha na asilimia 92 mwaka 1996) wameripoti kuwa wamepata angalau chanjo moja ya kuzuia pepopunda wakati wakiwa na mimba, asilimia 61 tu ndiyo wamepata chanjo mbili zinazopendekezwa. Kwa ujumla, asilimia 42 ya watoto wanaozaliwa na wanawake wanaoishi vijijini na asilimia 49 ya watoto wanaozaliwa na wanawake wasiokuwa na elimu hawakupata chanjo hiyo au wamepata chanjo moja na kuwafanya wasiwe na kinga ya pepopunda.

Huduma za kujifungua na baada ya kujifungua

Asilimia arobaini na nne ya watoto wachanga wanaozaliwa Tanzania wanazaliwa katika sehemu zitoazo huduma za afya, umeshuka kidogo kuanzia mwaka 1991-92 (asilimia 53) hadi mwaka 1996 (asilimia 47). Kuna tofauti muhimu kufuatana na mahali kina mama wanapoishi na kiwango cha elimu. Wengi wao (asilimia 83) wanaoishi mijini wanazalia kwenye sehemu zitoazo huduma za afya, kulinganisha na asilimia 53 wanaoishi vijijini. Wanawake wasiokuwa na elimu

Huduma kabla ya kujifungu, wakati wa kujifungua na baada



(asilimia 24) wana uwezekano mdogo wa kuzalia sehemu zinazotoa huduma za afya kuliko wanawake waliomaliza elimu ya shule za msingi (asilimia 51) au wenye elimu ya sekondari au elimu ya juu (asilimia 79).

Mahali pa kuzalia kunashawishi aina ya msaada ambao mwanamke anaweza kupata wakati wa kujifungua. Kwa mfano, kila wanawake watatu katika wanawake wanne wa mijini wanapata msaada wa daktari wakati wa kujifungua, nesi au mkunga, kulinganisha na mmoja kati ya wanawake wanne wa kijijini.

Kwa ujumla, ndugu na marafiki (asilimia 29) wanatoa msaada mwingi wakati wa kujifungua, wakifuatiwa na manesi na wakunga (asilimia 28) na wahudumu waliofunzwa (trained birth attendants) (asilimia 11). Asilimia ya wanaojifungua ambao wanasaidiwa na wafanyakazi waliofuzu imekuwa ikishuka kutoka mwaka 1991-92 (kutika asilimia 44 hadi asilimia 36 mwaka 1999).

Inapendekezwa kuwa wanawake wachunguzwe siku chache baada ya kujifungua, ili kugundua matatizo ya kiafya yanayoweza kutokea baada ya kujifungua. Asilimia kubwa (asilimia 38) ya wanawake wa Tanzania hawapati huduma ya baada ya kujifungua; zaidi ya hayo, ni nusu tu ambao wamechunguzwa katika kipindi cha siku mbili, tukichukulia ya kuwa wanawake wanaojifungulia katika sehemu zinazotoa huduma za afya wanachunguzwa baada ya kujifungua.

Madini joto kwenye chumvi na ziada ya vitamini A

Licha ya kuongezeka kwa hatari ya ukosefu wa lishe kunakosababisha matezi na kudumaa, halikadhalika, ukosefu wa akili na taahira, ukosefu wa madini joto kwenye chakula kuna sababisha vifo vya watoto wadogo na vile vile kukosa kupata mimba. Takwimu za utafiti huu zinaonyesha theluthi mbili ya kaya zinatumia chumvi yenye madini joto yanayotosheleza, kiwango hiki ni kikubwa kwa wanaoishi maeneo ya mjini (asilimia 86) kuliko maeneo ya vijijini (asilimia 60). Ni asilimia 9 tu ya kaya za Pemba ndizo zinazotumia chumvi yenye madini joto, kulinganisha na asilimia 52 ya kaya za Unguja na asilimia 68 ya kaya za Bara.

Lishe nyingine ndogo ndogo ambazo ni muhimu kwa wanawake ambao ndiyo kwanza wamejifungua ni vitamini A. Ni asilimia 12 tu ya kinamama ambao ndiyo kwanza wamejifungua wa Bara na asilimia 2 ya kinamama ambao ndiyo kwanza wamejifungua wa Zanzibar wanapata vitamini A ya ziada katika kipindi cha miezi miwili baada ya kujifungua.

Afya ya Mtoto na Maradhi

Chanjo za watoto

Watoto wanaopata chanjo wana uwezo mkubwa wa kuendelea kuishi kwa sababu wanajikinga na maradhi mengi yanayompata mtoto. Karibu watoto saba kati ya watoto kumi wa Kitanzania wenye umri wa miezi 12 - 23 wanachukuliwa kuwa wamepata chanjo zote kwa sababu wanakuwa wameshapata chanjo za BCG, surua, chanjo 3 za DPT na ya kuzuia kupooza (chanjo ya kupooza anayopata baada ya kuzaliwa); asilimia 5 hawakuweza kupata chanjo yoyote. Asilimia themanini na moja ya wanaoishi mjini wamepata chanjo zote, kulinganisha na asilimia 66 ya watoto wanaoishi kijijini. Watoto ambao mama zao hawana elimu (asilimia 50) wana uwezekano mdogo wa kukingwa na maradhi kuliko watoto ambao mama zao wamemaliza elimu ya msingi (asilimia 78). Chanjo za mwanzo ambazo ni za kuzuia kupooza (asilimia 93) na ya DPT (asilimia 92) ndizo ambazo zinatumika sana, marudio ya tatu ya chanjo hizo yameshuka hadi kufikia asilimia 80 na 81 kwa kila moja.

Ni asilimia ngapi ya watoto wamepata chanjo za kujikinga na magonjwa?



Matibabu ya watoto walio wahi kuumwa katika kipindi cha wiki 2 kabla ya utafiti
(watoto wenye umri chini ya miaka 5)

Matibabu ya magonjwa ya watoto

Kina mama ndiyo watunzaji wakubwa wa watoto, kwa hiyo ni muhimu kwao kungundua ishara za matatizo makubwa ya mtoto ili aweze kupatiwa huduma za haraka. Kati ya kina mama watatu kwa kila wanne wenye watoto wa umri chini ya miaka mitano Tanzania wameeleza aina mbili au zaidi ya ishara zinazoonyesha kuwa mtoto ana matatizo. Homa inayompata mtoto ndiyo ugonjwa mkubwa ambao umejitokeza kufahamika sana. Mtoto kuwa mgonjwa,

kupumua haraka haraka, au hanywi kama inavyotakiwa ni ishara za maradhi ambayo kina mama wanayatambua.

Magonjwa ya kuharisha na kupumua kwa tabu, halikadhalika homa ndiyo sababu kubwa zinazosababisha watoto kufariki. Katika kipindi cha wiki mbili kabla ya utafiti, asilimia 12 ya watoto wenye umri wa chini ya miaka mitano walipata kuharisha, wakati asilimia 14 walipata kukohoa ikiambatana na kupumua kwa haraka (acute respiratory infection - ARI) na asilimia 35 wamepata homa. Kati ya watoto waliokuwa wakiharisha na watoto waliokuwa na matatizo ya ARI au homa, wawili kati ya kila watoto watatu wamepelekwa kwenye sehemu zitoazo huduma za afya au mtoaji wa huduma ya matibabu.

Dalili za homa mara nyingi zinahusiana na ugonjwa wa malaria, kwa hiyo ni jambo la kufurahisha kuona kwamba nusu ya watoto wenye homa wamepewa dawa ya kutibu malaria. Njia nyingine ya kuwakinga watoto ili wasipate malaria ni kuhakikisha kuwa wanalala ndani ya vyandarua vilivyotiwa dawa ya kuzuia wadudu. Ni kaya moja kati ya kaya tano za Tanzania zilizoripoti kwamba watoto wote wa chini ya miaka mitano wamelalia chandarua usiku wa kuamkia siku ya mahojiano - kati yao, asilimia 10 wameeleza kuwa vyandarua havijawahi kutiwa dawa. Ingawa vyandarua vinatumika sana kwenye maeneo ya mijini kuliko maeneo ya vijijini, asilimia ya vyandarua vilivyotiwa dawa ni ile ile (asilimia 10).

Vifo vya watoto

Viwango vya vifo vya watoto wadogo Tanzania vinaonekana vimeongezeka kidogo tokea utafiti wa mwaka 1996. Hali ya vifo sasa hivi ni mtoto mmoja kati ya watoto saba (vifo 147 kwa watoto 1,000 waliozaliwa hai) watakufa kabla ya kutimiza umri wa miaka mitano. Kiwango cha vifo vya umri wa chini ya miaka mitano vilikuwa watoto 137 kwa kila watoto 1,000 mwaka 1996 na watoto 141 kwa kila watoto 1,000 mwaka 1991-92. Viwango ni vikubwa zaidi kwa maeneo ya vijijini (watoto 166 kwa kila watoto 1,000 mwaka 1999) ukilinganisha na maeneo ya mijini (watoto 144 kwa kila watoto 1,000), na ni chini zaidi kwa Zanzibar (watoto 114 kwa kila watoto 1,000). Kwa ujumla, theluthi mbili ya vifo vinatokea katika miaka mitano ya mwazo ya maisha (watoto 147 kwa kila watoto 1,000) kwa kweli vinatokea katika mwaka wa kwanza wa maisha (watoto 99 kwa kila watoto 1,000).

Vifo kwa wenye umri wa chini ya miaka mitano kwa mambo machache yaliyochaguliwa



Vifo kwa kila watoto hai 1,000 waliozaliwa

Njia muhimu ya kupunguza vifo hivyo ni kuhakikisha kuwa wazazi wanasubiri kwa muda ili kupata mtoto mwengine baada ya kuzaliwa aliyetangulia. Kwa mfano, vifo vya chini ya miaka mitano ni watoto 195 kwa kila watoto 1,000 waliozaliwa wakati muda wa mtoto aliyetangulia kuzaliwa ni chini ya miaka miwili, na vinashuka mpaka kufikia watoto 112 kwa kila watoto 1,000 kwa muda wa miaka minne au zaidi tokea azaliwe mtoto aliyetangulia, inayomaanisha kuwa hatari ya vifo ni pungufu kwa asilimia 43. Watoto waliozaliwa kwa wanawake wenye umri chini ya miaka 20 wako katika hatari kubwa ya kupoteza maisha kabla ya kufikia umri wa miaka mitano (watoto 227 kwa kila watoto 1,000) kuliko watoto waliozaliwa kwa wanawake wenye miaka ya 30 (watoto 166 kwa kila watoto 1,000).

LISHE

Kunyonyesha

Watoto wa Tanzania wananyonyeshwa titi la mama kwa muda mrefu (karibu miezi 20), lakini wanapewa vyakula vya ziada na maji ya kawaida mapema zaidi, jambo linalowafanya wawe katika hatari ya kupata maambukizo, kuharisha na kukosa kinga za maradhi kwa ujumla. Kumnyonyesha mtoto maziwa ya mama pekee, njia inayopendekezwa katika kipindi cha miezi minne au sita ya kwanza ya maisha ya mtoto, kiwango chake kiko juu katika mwezi mmoja wa kwanza (asilimia 58); kinashuka na kufikia asilimia 25 kwa watoto wa miezi miwili hadi mitatu na asilimia 16 tu kwa watoto wenye umri wa miezi minne hadi mitano. Kwa watoto wenye umri wa miezi minne mpaka mitano, asilimia 14 ya watoto hao wananyonyeshwa maziwa ya chupa, ni jambo jingine ambalo linahatarisha watoto kuambukizwa maradhi. Licha ya matokeo hayo, na kwa sababu ya programu za elimu zinazotekelezwa na serikali, zaidi ya nusu ya wanawake wanafahamu muda muafaka wa kunyonyesha mtoto maziwa ya mama pekee mpaka mtoto afikie umri wa miezi minne hadi sita.

Tabia ya kulishwa chakula na ongezeko la vitamini A kwa watoto wenye umri wa chini ya miaka 3



Hali ya lishe kwa watoto

Kiwango cha kudumaa kwa watoto Tanzania bado kipo juu kwa kipindi cha miaka kumi iliyopita. Matokeo ya utafiti wa 1999 yanaonyesha asilimia 44 ya watoto wenye umri chini ya miezi mitano wanachukuliwa kuwa ni wafupi kulingana na umri wao. Zaidi ya hayo, asilimia 29 ya watoto wana uzito ambao ni chini ya kiwango kinachotakiwa kulingana na umri wao; hali hiyo imebaki kama ilivyotokea mwaka 1991-92. Watoto wanaoishi maeneo ya vijijini (asilimia 48 wamedumaa) wana matatizo makubwa ya utapia mlo kuliko wanaoishi maeneo ya mijini (asilimia 26 wamedumaa). Kudumaa na kuwa na uzito mdogo kumejitokeza sana Bara kuliko Zanzibar.



Baada ya kila umri wa miezi sita, inapendekezwa watoto wapewe vyakula vya vitamini A au nyongeza ya vitamini A (supplements). Ni mtoto mmoja tu kati ya saba wenye umri wa miezi 6-59 wametolewa taarifa ya kuwa wamepata nyongeza ya vitamini A katika kipindi cha miezi sita kabla ya utafiti.

UKIMWI

Kufahamu namna ukimwi unavyoambukizwa

Inakisiwa kuwa idadi ya wagonjwa wa Ukimwi Tanzania inaongezeka haraka katika kipindi cha miaka ya hivi karibuni. Ugonjwa huu unafahamika sana duniani, na wanawake wengi wanajuwa kuwa kuna njia za kujikinga ili wasipate virusi hivyo. Njia ambayo inafahamika sana kujikinga na Ukimwi kwa wanawake na wanaume ni utumiaji wa mipira (asilimia 56 kwa wanawake na 71 kwa wanaume), kufanya mapenzi na mtu mmoja (asilimia 47 kwa wanawake na 48 kwa wanaume), kuacha kabisa kufanya mapenzi (asilimia 28 kwa wanawake na 31 kwa wanaume). Kwa ujumla, nusu ya wanawake wametaja njia zote tatu za kujikinga ili wasiambukizwe ukimwi, maeneo ya mijini wanafahamu zaidi kuliko maeneo ya vijijini. Zaidi ya hayo, karibu asilimia 80 ya wanawake wanafahamu kuwa vijidudu vya Ukimwi vinaambukiza kutoka kwa mama kwenda kwa mtoto, na karibu asilimia 70 wanafahamu kuwa mtu anaeonekana na afya nzuri anaweza kuwa ameambukizwa.

Kufahamu na kijikinga dhidi ya Ukimwi



Asilimia 36 ya wanawake na asilimia 41 ya wanaume wanaamini kuwa hawako katika hatari ya kuambukizwa Ukimwi, karibu robo ya wanawake na wanaume wana imani ndogo ya kuambukizwa. Sababu zinazofanya wanawake wafikiri kuwa na hatari kubwa ya kuambukizwa ni kuwa wenzao wana marafiki wengi (asilimia 55) au hawatumii mpira (asilimia 34); kwa wanaume, asilimia 25 wanafikiri wenzao wana marafiki wengi na asilimia 43 hawatumii mpira. Wanaume wanaamini zaidi kuwa wako kwenye hali ya hatari kuambukizwa kwa sababu wanao marafiki wengi (asilimia 34) kuliko wanawake (asilimia 8).

Kufahamu, kukubalika na kutumika mpira wa baba/mama

Wakati asilimia 92 ya wanawake na asilimia 96 ya wanaume ambao wameshawahi kukutana kimwili wanaufahamu mpira, lakini ni asilimia 8 ya wanawake na asilimia 16 ya wanaume wametumia mpira mara ya mwisho walipokutana kimwili. Utumiaji wa mpira na marafiki ambao siyo wa kawaida upo juu (asilimia 24 kwa wanawake na asilimia 34 kwa wanaume).

Nusu ya ya wananwake na asilimia 56 ya wanaume wanaamini kuwa inakubalika kwa wanawake kuwaambia wanaume watumie mpira. Ikiwa mwanaume anao ugonjwa wa zinaa, asilimia 55 ya wanawake na asilimia 58 ya wanaume wanaamini kuwa inakubalika kwa mwanamke kumuambia atumie mpira au akatae kufanya nae mapenzi.

Kupimwa ukumwi

Asilimia saba ya wanawake na asilimia 12 ya wanaume wamepimwa ukimwi Tanzania kufutana na matokeo ya utafiti. Kukiwa na wanawake wengi (asilimia 54) wanaopenda kupimwa na wanafahamu mahali pa kwenda (asilimia 52) kupimwa ukimwi, ukosefu wa kufahamu chanzo kwa ajili ya kupimwa (asilimia 35), kutokujua muda (asilimia 20) na gharama (asilimia 18) ndiyo tofauti kubwa zilizokuwepo.

MUHTASARI NA MAPENDEKEZI

Uzazi na uzazi wa mpango

Takwimu kutoka kwenye utafiti huu zinaonyesha kuwa viwango vya uzazi Tanzania vimeendelea kushuka, hata hivyo, kushuka kwake kumekuwa kwa taratibu na kiwango chake bado kiko juu kikiwa na wastani wa watoto watoto 5.6 kwa mwanamke mmoja, kinapitana na kiwango cha watoto 2.1 kwa mwanamke kinachotakiwa kuwa na idadi ya watu inayotakiwa kwa muda mrefu. Ingawa hii ina maana ya kuwa idadi ya watu katika nchi itaendelea kuongezeka kwa kiwango cha kasi, ingevumiliwa kama watoto wote hawa wangekuwa watoto wanaohitajika. Hata hivyo, takwimu za utafiti zinaonyesha kuwa kiwango kikubwa cha watoto wanaozaliwa hawakupangwa kuzaliwa- walitakiwa kuzaliwa baadae (asilimia 11) au hawakutakiwa kuzaliwa (asilimia 11). Kupunguza watoto wasiohitajika kuzaliwa kunahitaji bidii kubwa kuhakikisha kwamba wale wote ambao hawahitaji mtoto kwa muda huu wanapatiwa njia rahisi na ya kudumu ya uzazi wa mpango.

Takwimu za utafiti zinaonyesha kuwa wanawake na wanaume wameshasikia kuhusu aina mbali mbali za njia za uzazi wa mpango na kwamba upatikanaji wa taarifa za uzazi wa mpango umesambaa. Zaidi ya hayo, kukubalika kwa njia za uzazi wa mpango kunaonekana kuko juu, kukiwa na robo tatu ya wake na wanaume wote wakikubaliana na uzazi wa mpango. Inashangaza kuona kuwa kukataa kutumia - kwa baadhi ya waliohojiwa au yeye mwenyewe au mwenza wake - ni sababu ya pili kuu iliyoelezwa kutokuwa na nia ya kutumia njia za uzazi wa mpango maishani. Kwa kiwango fulani hii inatupatia mwangaza wa baadhi yao kukataa utumiaji wa uzazi wa mpango, bidii ya kuwaelimisha zaidi watumiaji muhimu kunaweza kusababisha wengi wao kuona kuwa njia za uzazi wa mpango ni bora kwao.

Matumizi ya uzazi wa mpango yanaendelea kukuwa, kukiwa na ongezeko kubwa kwa njia ya sindano, hivi sasa ni njia inayotumika sana kwa wanawake. Bidii katika eneo hili iegemee zaidi kwenye kuongeza matumizi ya njia za muda mrefu kama kufunga kizazi na kitanzi kwa wanawake ambao wanasema hawataki tena watoto.

Mama na afya ya mtoto

Takwimu zinaonyesha kuwa kumekuwa na ongezeko la watoaji wa huduma za kabla ya kujifungua zinazotolewa na manesi, wakunga na wasaidizi wa afya. Uchunguzi wa kuwa jambo hili linaweza likawa sababu ya kushuka kwa ubora wa huduma linaweza kusaidia.

Jambo jingine linalosumbua ni kupungua kwa watoto wanaozaliwa katika sehemu zitoazo huduma za afya. Hii inasababisha watoto wachache wanaozaliwa ndiyo wananosaidiwa na wafanyakazi wa afya waliofuzu, kukiwa na ongezeko la hatari ya magonjwa na vifo. Uchunguzi zaidi unahitajika katika eneo hili ili kufahamu sababu zinazoweza kupunguza zaidi watu wasiozalia kwenye huduma za afya.

Utafiti huu unaonyesha kuwa kupunguwa kwa vifo vya watoto wadogo kulikojionesha hapo awali kumebakia kama ilivyokuwa. Ingawa sababu kuhusu suala hili haziko wazi, ukimwi unaweza kuchangia. Takwimu zinaonesha kuwa chanjo za watoto hazikuongezeka, halikadhalika, kunyonyesha maziwa ya mama na hali ya lishe kama ilivyojitokeza kwa kupima urefu na uzito. Eneo moja ambalo linaweza kupunguza vifo vya watoto wadogo ni kuwapatia nyongeza ya vitamini A; utafiti unaonesha kuwa asilimia 14 ya watoto waliolengwa wanapatiwa huduma hii.

Ukimwi

Takwimu za utafiti huu zinaonyesha kuwa bidii ya kuwaelimisha wanawake na wanaume kuhusu ukimwi zimekuwa na mafanikio; wote wamesikia kuhusu ukimwi na wengi zaidi wanafahamu ukimwi unaambukiza. Zaidi ya hayo, utumiaji wa mpira umeongezeka kwa wapenzi wasio wa kawaida kwa wanawake, ingawa siyo hivyo kwa wanaume. Bidii inahitajika kuongezwa kwa njia salama za kufanya mapenzi ambako kunaweza kusaidia kupunguza kuongezeka kwa ugonjwa huu. Kuongeza upatikanaji wa kupimwa Ukimwi na kuwashawishi wanawake na wanaume kupimwa kunaweza kusaidia.